**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

---

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

# TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

---

Ofisi ya Bunge,
Idara ya Kamati za Bunge,
S. L. P. 941,
**DODOMA**

**21 Mei, 2018**

**YALIYOMO**


**SEHEMU YA KWANZA ........ 1**

**MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA ........ 1**

**1.0 UTANGULIZI ........ 1**

**SEHEMU YA PILI ........ 4**

**2.0 UCHAMBUZI WA MAJUKUMU YALIYOTEKELEZWA ........ 4**

2.1 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WABAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 ........ 4

2.2 UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 ........ 4

2.3 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 ........ 5

2.4 MATOKEO YA UKAGUZI WA BAADHI YA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018 ........ 6

2.5 MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 ........ 7

2.6 UTEKELEZAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 ........ 9

2.7 MPANGO WA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 13

2.8 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 ........ 14

2.9 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 ........ 14

2.10 MASUALA MENGINE MUHIMU YALIYOJITOKEZA WAKATI WA KUCHAMBUA NA KUPITISHA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HII KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 ........ 15

**SEHEMU YA TATU ........ 21**

**3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI ........ 21**

3.1 SEKTA YA UTALII ........ 21

3.2 SEKTA YA WANYAMAPORI ........ 22

3.3 SEKTA YA MALIKALE ........ 23

3.4 MAKUMBUSHO YA TAIFA ........ 23

3.5 SEKTA YA MISITU NA NYUKI ........ 24

**4.0 HITIMISHO ........ 26**

## SEHEMU YA KWANZA

## MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** Fasili ya 7 (1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 inataja majukumu ya Kamati za kudumu za Bunge za kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na utalii kuwa ni :-

(a) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia (Wizara ya Maliasili na Utalii);
(b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya wizara hii;
(c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za wizara hii; na
(d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu mengine yaliyoorodheshwa hapo juu, Kanuni ya 98(1),(2), ya kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo 2016 imeweka sharti la Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa bajeti ya wizara inazozisimamia. Naomba kutoa taarifa kuwa tarehe 15 hadi 18

Machi, 2018 Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Aidha kati ya tarehe 27 hadi 28 Machi,2018 Kamati ilichambua Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa**- fungu 69.**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa ufafanuzi wa mambo manne yafuatayo:-

(a) Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa maendeleo na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ikijumuisha;-

(i) Makusanyo ya Mapato 2017/18;

(ii) Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(iii) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(iv) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

(b) Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; ukijumuisha.

(i) Makisio ya Makadirio ya Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

(ii) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

(iii) Mambo mengine muhimu yaliyojitokeza wakati wa kuchambua na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

(c) Maoni na Ushauri wa Kamati;

(d) Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa maelezo yanayotolewa katika taarifa hii ni masuala yaliyo halisi; na ushauri uliotolewa ni kwa ajili ya kuleta tija katika sekta ya maliasili na Utalii. Hivyo, ni matumaini ya Kamati kwamba maoni na ushauri wa kamati vitatiliwa maanani na kutekelezwa.

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJUKUMU YALIYOTEKELEZWA

## 2.1 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WABAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, Mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 yalijikita zaidi katika makusanyo ya maduhuli, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa hususan fedha za matumizi mengineyo (OC) na fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kamati ilichambua hali halisi ya makusanyo ya maduhuli, kwa kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele yake. Aidha kamati ilitafakari majadiliano yaliyofanyika kisha kufikia hatua ya kutoa maoni na mapendekezo.

## 2.2 UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara ilitarajiwa kukusanya maduhuli ya kiasi cha Shilingi **21,289,283,007.50** kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato yanayotokana na sekta ya Maliasili na Utalii. Hadi kufikia Februari 2018, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni **13,018,796,471.23** sawa na asilimia 61 ya kiwango kilichokadiriwa kukusanywa kwa mwaka, hii ni ongezeko la asilimia **5.6** la makusanyo ikilinganishwa na kipindi kama hichi kwa Mwaka wa Fedha uliopita.

**Mheshimiwa Spika** Mwenendo wa makusanyo pamoja na ongezeko hilo hauridhishi, na kwa hali hiyo Wizara inaweza kutofikia malengo yake kikamilifu. Kamati inaona kuwa endapo utalii utapewa kipaumbele na kuboreshwa ipasavyo Wizara itaweza kukusanya zaidi na kuchangia vizuri kwenye pato la Taifa.

## 2.3 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, Uwiano na upatikanaji wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara, miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo hadi kufikia februari 2018, kwa mwaka wa fedha 2017/18 unaonyeshwa kwenye **jedwali Na. 1**

**Jedwali Na.1 Upatikanaji Fedha za Matumizi ya Kawaida, Miradi ya Maendeleo na Mishahara**

| NA | MAELEZO | FEDHA ZILIZOIDHINISHWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 | FEDHA ZILIZOTOLEWA HADI FEBRUARI, 2018 | ASILIMIA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mishahara &Matumizi Mengineyo | 96,793,662,000.00 | 36,536,164,379.00 | 38% |
| 2 | Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo | 33,803,284,000.00 | 11,353,250.489.00 | 33.5% |
| 3 | Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo | 18,000,000,000.00 | 16,593,530,813.00 | 92% |

***Chanzo:Taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Maliasili na Utalii 2017/2018***

**Mheshimiwa Spika, C**hangamoto ya ucheleweshaji wa utolewaji wa fedha kwa wakati hususani fedha za ndani imekuwa ikiathiri sana utekelezaji wa miradi na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo ya wizara.

## 2.4 MATOKEO YA UKAGUZI WA BAADHI YA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Mradi uliokaguliwa ni mradi namba **4810** wa kujenga uwezo wa Mapori ya Akiba na kikosi dhidi ya Ujangili (***capacity building in Game Reserves and Anti-Poaching unit in Tanzania***) uliotekelezwa katika Mapori yote ya Akiba nchini. Aidha Kamati ilipata fursa ya kukagua utekelezaji wa mradi huu katika Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi na Kimisi.

**Mheshimiwa Spika,**Kamati ilielezwa kuwa mradi wa kujenga uwezo katika Mapori ya Akiba yaani ( Capacity Building in Game Reserves and Anti-poaching Unit in Tanzania) ulianza kutekelezwa katika mwaka wa Fedha 2014/2015 lengo likiwa ni kujenga uwezo wa kusimamia Maliasili kwa kuzingatia mpango Mkakati wa kupambana na ujangili ambao ulizinduliwa mwezi Mei,2014.

Mradi huu ulikusudiwa kutekelezwa kwa kutumia fedha za ndani ambapo ulitazamiwa kugharimu Shilingi **2,158,350,000** kwa miaka mitatu yaani 2014/2015-2017/2018. Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa mradi ni wa kusuasua kwakuwa tangu kuzinduliwa kwake hakuna fedha zozote za ndani zilizopelekwa na badala yake unategemea zaidi fedha za wafadhili kutoka nje hali itakayopelekea mradi kutokuwa endelevu. Aidha kamati ilibaini uharibifu mkubwa wa mazingira uliosababishwa na uvamizi wa mifugo katika mapori haya pamoja na shughuli nyingine za binadamu.

**Mheshimiwa Spika**, Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi na Kimisi yana ukubwa wa kilomita za mraba 4,702 na yana wafanyakazi 68 tu! Hali inayosababisha tatizo la uvamizi kuwa kubwa kutokana na idadi

ndogo ya wafanyakazi iliyopo. Kamati inaipongeza Serikali hususan kamati za ulinzi na usalama ya Mkoa na zile za wilaya zote za Mkoa wa Kagera kwa kuendesha operesheni maalum ya kuondoa mifugo katika Mapori haya na kusababisha uoto wa asili na wanyamapori walioanza kutoweka kurejea katika Mapori haya. Kamati inaishauri Serikali kufanya doria za mara kwa mara katika mapori haya ili kuhakikisha kuwa uvamizi hautokei tena.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwepo kwa miundombinu mibovu ya barabara, uchache na uchakavu wa magari ya kufanya doria,hali duni ya makazi ya watumishi pamoja na uhaba wa watumishi hali inayofanya kazi ya kudhibiti uvamizi wa mapori kuwa ngumu. Kutokuwepo kwa barabara katika pori la Kimisi kwenye mpaka wa Tanzania na Rwanda kunazuia ulinzi kwenye mpaka huu hali inayowapa urahisi wavamizi kufanya ujangili wa wanyamapori, misitu na uvuvi katika maeneo yaliyo ndani ya nchi yetu kwa urahisi.

## 2.5 MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ni kujiridhisha na uwepo wa miradi na matumizi ya fedha zilizoidhinishwa sawia na miradi husika ili kuwa katika nafasi nzuri ya kuishauri Serikali ipasavyo**.** Kutokana na hali iliyoonekana katika ukaguzi wa miradi na kutokana na taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilizowasilishwa, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(a) Utekelezaji wa miradi ya maendeleo hauridhishi kutokana na kasi ndogo ya upatikanaji wa fedha. Hadi kufikia Februari 2018 miradi mingi haikupata fedha zilizoidhinishwa kuweza

kutekeleza miradi husika. Hali hii haina tofauti ikilinganishwa na hali ya bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017.

(b) Kutopeleka fedha katika miradi kwa wakati kunaathiri mwenendo mzima wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, uchambuzi wa taarifa za miradi unaonyesha kuwa hata kwa miradi iliyotengewa fedha za ndani haikupelekewa fedha kwa wakati kama ilivyokusudiwa.Aidha kwa ile iliopelekewa fedha hizo kiwango kilichotolewa ni kidogo sana, hadi februari 2018,Wizara ilipokea kiasi cha shilingi **11,353,250.489** kati ya **33,803,284,000** cha fedha za ndani sawa na asilimia 33.5% na shilingi **16,593,530,813** kati ya **18,000,000,000** fedha za nje sawa na asilimia 92%. Hali inaonyesha wazi kwamba utekelezaji wa miradi kwa kutumia fedha za ndani hauridhishi.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi uliofanywa na kamati, utekelezaji wa miradi ya maendeleo hauridhishi. Hadi kufikia Februari, 2018 kati ya miradi 12 iliyopangwa kutekelezwa miradi 4 haikupelekewa fedha kabisa. Miradi hiyo ni **Utalii House Phase II** mradi **Na-6367 ,Construction of Theme park** mradi **Na-5202, Capacity Building in Game reserves and Anti-Poaching Unit in Tanzania** mradi Na **-4810 na capacity building in Forestry and Bee keeping Mradi Na 4648.**

Kwa utaratibu huu inatia shaka dhamira yaSerikali kutekeleza miradi ya maendeleo na kwa vyovyote vile haiwezi kufikia malengo yake kama ilivyokusudia.

## 2.6 UTEKELEZAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa yapo maoni yaliyofanyiwa kazi kikamilifu, yapo maoni yanayoendelea kufanyiwa kazi, lakini yapo maoni ambayo hayakufanyiwa kazi kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha miundombinu ya utalii hususan barabara, huduma za maji na umeme ambavyo vimeendelea kuvutia watalii wengi kutembelea vivutio vya utalii na kuongeza idadi ya watalii hapa nchini, Aidha Serikali inaendelea na maboresho na upanuzi wa viwanja vya ndege kama J.K. Nyerere na KIA ambavyo vitasaidia kuvutia mashirika ya ndege kutua na kuongeza idadi ya watalii hapa nchini. Kamati inaipongeza Serikali kuwezesha kujengwa kwa uwanja wa ndege wa Chato. Uwanja huu utasaidia kufungua fursa nyingi za utalii hasa vivutio vilivyoko katika kanda ya ziwa. Vivutio hivyo ni pamoja na Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda, Rumanyika, Hifadhi za Taifa za Saanane na Rubondo n.k. Ili kuupa thamani uwanja wa ndege wa Chato ni muhimu Serikali ikawekeza vya kutosha katika kuviendeleza vivutio vya utalii vya ukanda huu,kujenga na kuimarisha miundombinu ya barabara,maji umeme pamoja na kuvutia wawekezaji kujenga mahoteli  ili kuvutia watalii wengi zaidi kutembelea vivutio vyetu katika kanda ya ziwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na migogoro mingi ya mipaka baina ya wananchi wanaopakana na maeneo

yaliyohifadhiwa na Mamlaka zinazosimamia hifadhi hizo. Kamati imetoa ushauri jinsi ya kumaliza migogoro hiyo lakini bado migogoro ipo na mingine inaongezeka. Serikali imechukua hatua hatua mbali mbali za kutatua migogoro hiyo zikiwemo Kamati na Tume mbali mbali zilizoundwa na Waziri Mkuu kushughulikia migogoro lakini bado migogoro inaendelea kuwepo na mingine kuongezeka. Hivi sasa Serikali inaeendesha zoezi la kuweka vigingi katika mipaka ya hifadhi jambo ambalo limepingwa na wananchi hadi kusababisha Serikali kutumia nguvu nyingi kupita kiasi ikiwemo matumizi ya silaha kutekeleza zoezi hilo. Kamati inaona moja ya changamoto kubwa inayosababisha migogoro kuendelea ni serikali kuweka mipaka bila ya kuwa na ushirikishwaji mpana wa wananchi. Katika hali ya kusikitisha vigingi vingine vimewekwa katika maeneo ya shule na vingine ndani ya nyumba za watu! **Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-**

i) **Serikali isitishe mara moja zoezi la kuweka vigingi katika mipaka ya Hifadhi.**

ii) **Serikali ifanye tathmini mpya ya maeneo yote yaliyohifadhiwa na kubainisha mipaka yake. Zoezi hili liwe na ushirikishwaji mpana wa wananchi, viongozi wa wananchi na wadau wengine ili kupata muafaka wa pande zote.**

iii) **Serikali ibainishe maeneo yote ambayo bado yana sifa ya kuendelea kuhifadhiwa na ambayo hayana mgogoro ili mipaka yake ibainishwe kwa kuwashirikisha wananchi na**

**yale ambayo yamepoteza sifa ya kuwa hifadhi yapangiwe matumizi mengine.**

**iv) Serikali ijipe muda (Time Frame) wa kumaliza migogoro hiyo vinginevyo Serikali itaendelea kuunda Tume na Kamati mbali mbali bila kumaliza tatizo. Aidha ushauri unaotolewa na Kamati/Tume zilizoundwa uzingatiwe na kutolewa maamuzi.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hairidhishwi na namna Serikali inavyotoa takwimu za utalii. Mathalani takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya watalii imeongezeka kutoka 1,284,279 mwaka 2016 hadi kufikia 1,327,143 mwaka 2017 lakini takwimu hizo hazichanganui watalii wangapi walikuja nchini kwa ajili ya mapumziko katika hifadhi zetu jambo ambalo halitoi picha halisi ya mwenendo wa ukuaji wa sekta hii. Takwimu zinaonyesha kwamba idadi ya watalii iliongezeka kutoka watalii 1,137,182 hadi 1,284,279 mwaka 2015-2016 sawa na ongezeko la asilimia 12.9 ikilinganishwa na ongezeko la kutoka watalii 1,284,279 hadi watalii 1,327,143 mwaka 2016-2017 sawa na ongezeko la asilimia 3.3. Ongezeko hili ni chini ya wastani wa ongezeko la watalii kwa nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara ambao ni asilimia 7 kwa mwaka na pia ni nyuma ya nchi jirani ya Kenya ambayo idadi iliongezeka kwa asilimia 9.8.

Aidha, Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilieleza kuwa mapato yatokanayo na utalii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 yameongezeka kutoka dola za kimarekani billion 2.1 hadi billion 2.3 . Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, ongezeko hilo limechangiwa na utozaji wa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa huduma za utalii ambapo ilikuwa haitozwi katika miaka ya nyuma. Kwa takwimu hizi ni dhahiri kwamba

ukuaji wa sekta ya utalii kimapato na kiidadi inatia shaka kama kweli utalii unakua.

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 17 Machi, 2016 Serikali ilisitisha biashara ya wanyamapori hai nje ya nchi na kusababisha hali ya taharuki kwa wafanyabiashara hao. Chama cha wasafirishaji wanyamapori hai nje ya nchi yaani (***Tanzania Wildilife Exporters Association-TWEA*** ) kilitoa malalamiko yake kwamba wakati Serikali ikisitisha biashara hiyo, wafanyabiashara hawa walikuwa wamechukua mikopo benki, wamelipia leseni na tozo mbali mbali za Serikali, wamekamata wanyamapori na kuendelea kuwatunza kwa gharama kubwa wakisubiri kuwasafirisha. Serikali imechukua hatua mbali mbali katika kushughulikia malalamiko hayo. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na ahadi ya Waziri wa Maliasili na Utalii aliyoitoa tarehe 24 Mei, 2017 Bungeni wakati akihitimisha hoja ya bajeti ya wizara kwa mwaka wa fedha 2017/18. Ahadi ya Waziri ilikuwa kwamba, Serikali italipa fidia ya gharama walizotumia wafanyabiashara hao kulipia leseni na tozo mbali mbali pamoja na kuruhusu biashara hiyo iendeleee ndani ya mwaka mmoja kuanzia siku ya Tamko. Fidia hii bado haijalipwa na Jambo hili limechukua muda mrefu na limesababisha mateso makubwa kwa wafanyabiashara hao. **Kamati inashauri Serikali iharakishe kuwalipa fidia zao ili waweze kujikimu kimaisha. Kamati inaitaka Serikali itekeleze ahadi yake iliyotoa hapa Bungeni mwaka jana ya kuwaruhusu wafanyabiashara hawa kuendelea na biashara zao.**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilitekeleza ushauri wa Kamati kwa kuchukua hatua za kubainisha maeneo mapya yenye vivutio vya utalii katika mikoa ya Singida, Katavi, Rukwa, na Tabora kwa lengo la kuendeleza vivutio hivyo ili vivutie watalii na kuongeza pato la Taifa. Kamati inashauri kuwa zoezi hili liwe endelevu katika mikoa mingine

hapa nchini hasa mikoa ya kusini, nyanda za juu kusini na kanda ya Ziwa.

**Mheshimiwa Spika,** Biashara ya utalii inahitaji ushindani mkubwa utakaosaidiwa na ubunifu wa aina mbalimbali hususan matangazo *(Promotion).* Japokuwa matangazo haya ni gharama inasikitisha kuona kwamba Serikali imeendelea kutoa fedha kidogo kwa ajili ya uendeshaji shughuli za kitalii ambazo hazitoshelezi kutengeneza matangazo yanayokidhi ili kuendana na ushindani. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuongeza fedha kwa Bodi ya Utalii ili iweze kuutangaza utalii ndani na nje ya nchi yetu. Aidha Kamati inaishauri Bodi ya Utalii kuwapunguzia tozo wawekezaji waliojitolea kuvitangaza vivutio vyetu vya utalii kwa gharama zao ili iwe motisha kwa wao kuendelea kuisaidia nchi kwa kutangaza utalii wetu.

## 2.7 MPANGO WA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

a) Kutatua migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya hifadhi na wananchi

b) Kuboresha vivutio na kutangaza utalii;

c) Kukamilisha mkakati wa usimamizi wa pori Tengefu la loliondo

d) Kusimamia biashara ya wanyamapori hai

e) Kupandisha hadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

## 2.8 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

## MAKISIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya shilingi **24, 727, 240,073/=** kutokana na vyanzo mbali mbali**.** Kiasi hiki ni nyongeza ya shilingi **3,437,957,006/=** ikilinganishwa na shilingi **21,289,283,007/=** zilizokadiriwa kukusanywa Mwaka wa Fedha 2017/2018. **Ni mapendekezo ya Kamati kwamba Serikali ihakikishe inatafuta vyanzo vipya na mbinu bora zaidi za ukusanyaji wa mapato ili kuongeza mapato ya Sekta ya Maliasili na Utalii.**

## 2.9 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika**, Kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Maliasili na Utalii inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi **115,794,740,000**. Kati ya fedha hizo shilingi **85,816,658,000/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **29,978,082,000**/= kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa ujumla bajeti inayoombwa iimepungua kwa asilimia 22.1 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2017/2018.Aidha bajeti ya maendeleo imepungua kutoka shilingi **bilioni 51,803,284,000/** mwaka 2017/2018 hadi shilingi **bilioni 29,978,082,000/** mwaka 2018/2019 sawa na upungufu wa asilimia 42. Kwa bajeti hii ni dhahiri kwamba shughuli za uhifadhi zitaathirika. **Kamati inaishauri Serikali kuruhusu Taasisi za uhifadhi kama TANAPA, TFS, NCAA na TAWA kubakiza fedha (Retention) kwa ajili ya kuendeleza uhifadhi badala ya fedha zote kupelekwa mfuko mkuu wa HAZINA na kusubiri mgawo**

**ambao uzoefu unaonyesha kuwa pesa hizo hazipelekwi kwa wakati ama kutopelekwa kabisa.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hairidhishwi kabisa na mwenendo wa Serikali wa kupunguza bajeti ya wizara kwa mwaka 2018/2019 hali inayoashiria kwamba wizara itashindwa kufikia malengo yake hasa shughuli za uhifadhi. Aidha hata kwa ile miradi inayoidhinishiwa fedha za ndani hazipelekwi kwa wakati au hazipelekwi kabisa mfano miradi namba 5202 Construction of Theme Park na 6367 Utalii House Phase II haijapelekewa fedha kwa miaka minne mfululizo na kusababisha mdororo wa utekekezaji wa miradi hiyo. Kamati inahoji kuna haja gani ya kutenga fedha wakati Serikali ina hakika haitapeleka fedha hizo? Kama miradi hii haina umuhimu kwa taifa ni bora ikaondolewa katika bajeti kuliko kuiweka na kuitengea fedha na kusababisha bajeti kuonekana kubwa wakati haitatekelezwa.

## 2.10 MASUALA MENGINE MUHIMU YALIYOJITOKEZA WAKATI WA KUCHAMBUA NA KUPITISHA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HII KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika**, kulikua na maswala mbalimbali yalijitokeza wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii, hali ambayo iliilazimu Kamati kuiagiza Wizara kuleta Taarifa maalum tano kama ifuatavyo:-

i) Mgongano wa kisheria kati ya sheria mbali mbali za uhifadhi na sheria nyingine
ii) Athari za kutoza kodi ya ongezeko la thamani katika huduma za utalii
iii) Hali ya uendeshaji wa Jumuiya za hifadhi za wanyamapori (***Wildlife Management Areas- WMA's***)

iv) Hali ya migogoro kati ya maeneo yaliyohifadhiwa na wananchi wanaopakana na hifadhi hizo;na
v) Hali ya uwindaji wa kitalii.

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na mgongano wa kisheria kati ya Sheria mbali mbali za Uhifadhi na sheria nyingine kwa mfano Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 na Sheria ya Serikali za Mitaa, Tawala za Wilaya namba 7 ya Mwaka 1982 ambapo baadhi ya vijiji vimesajiliwa ndani ya maeneo ya hifadhi kinyume na Sheria ya Uhifadhi ambayo inakataza shughuli za kibinadamu ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa. **Kamati inaishauri Serikali kuhuisha sheria mbali mbali za uhifadhi ili ziendane na wakati uliopo. Aidha wakati wa kuhuisha sheria hizo izingatie vipengele vinavyoleta ukinzani kati ya sheria za uhifadhi na sheria nyingine ili vifanyiwe marekebisho stahiki.**

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 38 cha Sheria ya uhifadhi wa Wanyamapori namba 5 ya mwaka 2009 kimeweka masharti ya ugawaji vitalu vya uwindaji ikiwa ni pamoja na uhai wa leseni za uwindaji na utaratibu wa kuhuisha (***renew***) leseni za umiliki wa kitalu baada ya muda wake kuisha. Kumekuwa na sintofahamu baina ya wawekezaji na wamiliki wa vitalu vya uwindaji kwa upande mmoja na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa upande mwingine kutokana na barua na matamko mbali mbali yaliyotolewa na Wizara kuhusu uhai wa leseni zao kama ifuatavyo:-

i) Tarehe 13 Agosti, 2015 Wizara iliwaandikia wamiliki wa vitalu barua ya tathmini kuhusu utendaji wao na kwamba wanaweza kuomba kuhuisha muda wa leseni zao

ii) Tarehe 16 Januari, 2017 Wizara iliwaandikia barua wamiliki wa vitalu ikiwajulisha kuongezewa muda wa leseni zao kwa miaka mitano kuanzia Januari 2018 hadi Desemba , 2022

iii) Tarehe 23 Oktoba , 2017 Wizara ilitoa tamko la kufuta leseni zote za umiliki wa vitalu

iv) Tarehe 29 Desemba, 2017 Wizara iliwaandikia barua wamiliki wa vitalu kuwajulisha kuwa wameongezewa muda wa miaka miwili kuendelea na shughuli zao.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi unaonesha kuwa, Tamko la tarehe 23 Oktoba, 2017 pamoja na barua ya tarehe 29 Desemba, 2017 zimetolewa kinyume cha sheria ya Wanyamapori namba 5 ya mwaka 2009 pamoja na kanuni zake ambazo zimeweka bayana utaratibu wa kumilikishwa kitalu cha uwindaji na utaratibu wa kufutiwa leseni kwa anayekiuka masharti. Aidha Kifungu cha 38(8) cha Sheria ya uhifadhi wa wanyamapori, kimeeleza wazi uhai wa leseni za kumiliki kitalu ni miaka mitano (5). Kamati inaona hatua ya Wizara kuwaongezea miaka miwili (2) wamiliki wa vitalu ni kinyume cha Sheria na kanuni zilizopo.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii siyo tu imewavunja moyo wawekezaji wa kuendeleza uhifadhi katika vitalu bali pia imeikosesha serikali mapato kwani zaidi ya vitalu 18 vimerudishwa katika kipindi hiki na kufanya jumla ya vitalu vilivyo wazi kuwa 81 kati ya vitalu 159. **Kamati inaitaka Serikali kurejesha utulivu katika Tasnia hii kwa kuzingatia barua yake ya kuhuisha leseni za vitalu vya uwindaji ya Tarehe 16 Januari, 2017 vinginevyo sekta hii itaendelea kudorora na kuikosesha serikali mapato.**

**Mheshimiwa Spika** kumekuwepo na uharibifu wa vyanzo vya maji katika hifadhi zetu unaosababishwa na wafugaji kupeleka mifugo katika hifadhi hizo kwa lengo la kutafuta maji na malisho ya mifugo pamoja na

shughuli nyingine za kibinadamu. **Kamati inashauri Serikali kuchimba visima, mabwawa na malambo katika vijiji vyote vinavyozunguka hifadhi kwa lengo la kusaidia kuzuia wafugaji kupeleka mifugo katika vyanzo vya maji vilivyo katika hifadhi zetu. Serikali itekeleze ahadi yake ya kuwatengea wafugaji maeneo ya malisho ya mifugo ikiwa ni pamoja na kujenga miundombinu muhimu kwa mifugo.**

**Mheshimiwa Spika** kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa misitu hasa misitu inayomilikiwa na vijiji na Serikali za mitaa ambayo inakadiriwa kuchukua zaidi ya asilimia 52 ya eneo lote la misitu hapa nchini. **Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kudhibiti ujangili wa misitu ili kuinusuru na kuiepusha nchi yetu na madhara yatokanayo na uharibifu wa misitu. Aidha Kamati inaishauri Serikali Kuanzisha Mamlaka moja itakayokuwa na nguvu ya kisheria ya kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu yote hapa nchini. Wakala wa Misitu inasimamia misitu ya Serikali tu lakini haina udhibiti wa misitu inayomilikiwa na vijiji na Serikali za Mitaa.**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na ongezeko la watu na mifugo katika hifadhi hususan Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro wanaosababisha kuongezeka kwa gharama za matumizi yanayotolewa na Mamlaka ya Hifadhi na kupelekea Mamlaka hii kubeba mzigo mkubwa na gharama kubwa kuliko ilivyokadiria. **Kamati inashauri Serikali kuhuisha Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ili iendane na wakati. Aidha ufanyike utafiti wa faida na athari za uhifadhi mseto unaoendelea katika hifadhi hii ili kuendeleza hifadhi na kudumisha sifa yake ya kuwa eneo la urithi wa dunia.**

**Mheshumiwa Spika,** Mwaka 2016, serikali ilipitisha sheria ya VAT ambayo pamoja na mambo mengine ilianzisha utaratibu wa kutoza kodi ya ongezeko la thamani(VAT) katika huduma za utalii hali ambayo ilitarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwavile wadau hawakuwa wameshirikishwa mapema. Taarifa ya Serikali inaonyesha kuwa mapato hayajashuka kutokana na kutoza **VAT** katika huduma za utalii.**Kamati inaona ni mapema mno kwa Serikali kutoa hitimisho ya athari ya tozo hio kwa huduma za utalii. Kamati inashauri kwamba ni vema Serikali ifanye utafiti wa kutosha kuhusu athari za VAT katika huduma za kitalii. Aidha Serikali iongeze vigezo vitakavyotumika kupima mwenendo wa ukuaji wa Sekta ya Utalii kwa lengo la kubaini maeneo yenye upungufu na kuyafanyia marekebisho badala ya kutumia kigezo cha mapato na idadi ya watalii pekee.**

**Mheshimiwa Spika,** Kumekuwepo na changamoto katika uendeshaji na usimamiaji wa Jamii za uhifadhi wa Wanyamapori (WMA's). Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na baadhi ya Kanuni za uendeshaji wa Jamii za Uhifadhi wa Wanyamapori kupitwa na Wakati, kutokuwa na mfumo mmoja wa uendeshaji wa WMA's, Sekretarieti za WMA's kukosa utaalamu, Wanachama kutegemea wafadhili na WMA's kuingiliwa na mamlaka nyingine katika uendeshaji wake. **Kamati inashauri kuwa kanuni zilizoanzisha WMA's zipitiwe upya na kuhuishwa kwa lengo la kuzipatia WMA's nguvu na mamlaka za kisheria za kuendesha jamuiya hizi kwa ufaanisi zaidi. Aidha viongozi wa sekretarieti wawe na sifa za kitaaluma za kuongoza WMA's kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kuongoza jumuiya hizi. Vile vile Serikali iweke mfumo mmoja wa uendeshaji wa WMA's**

**na kwamba zisiingiliwe na mamlaka nyingine katika uendeshaji wake.**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) pamoja na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro zinachangia asilimia kumi na tano (15%) ya mapato ghafi kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali na asilimia tatu (3%) kwenda Mfuko wa Uendelezaji Utalii. Mapato haya kiutaratibu ni ya Serikali na Mashirika haya hayastahili kuyalipia kodi. Hata hivyo TRA imekuwa ikitoza kodi ya asilimia 30 (30%) ya mapato kwenye mashirika haya kitu ambacho si sahihi. Pamoja na mashirika hayo kuomba kodi hiyo iondolewe bado TRA imeendelea kutoza kodi. **Kamati inaishauri Serikali kuielekeza TRA kutotoza kodi kwenye mapato hayo kwani kodi hiyo inayaongezea mashirika hayo mzigo mkubwa na kuyafanya yashindwe kutekeleza baadhi ya majukumu yake ya msingi likiwemo jukumu kuu la uhifadhi.**

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nitoe maoni na ushauri wa Kamati kwa sekta mbalimbali zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo;-

### 3.1 SEKTA YA UTALII

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Utalii inazo fursa nyingi ambazo zikitumiwa kikamilifu zitaongeza mchango wake katika pato la Taifa.Kwa sasa Sekta hii inachangia asilimia 17 tu ya pato la Taifa. Ili kuongeza pato la Taifa kupitia Sekta ya Utalii, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo;-

a) Kuvibaini vivutio zaidi vya utalii vilivyoko nchini na kuviendeleza;

b) Kuwekeza miundombinu kwenye vivutio vya utalii kwa kuimarisha au kujenga barabara, viwanja vya ndege, mahoteli, maji, vyoo n.k ili kuvutia watalii kufika kwenye vivutio hivyo kwa urahisi;

c) Kupitia upya tozo mbali mbali zinazotozwa katika huduma za utalii na kuziondoa zile zinazoifanya Tanzania kuwa ghari zaidi ikilinganishwa na washindani wetu;

d) Kutenga fedha za kutosha pamoja na kuhamasisha bodi ya utalii kupitia wizara hii kuongeza ubunifu katika kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi ili kuendana na ushindani uliopo katika sekta ya utalii;na

e) Kushirikisha sekta binafsi katika uboreshaji na utangazaji wa vivutio vya utalii

## 3.2 SEKTA YA WANYAMAPORI

**Mheshimiwa Spika**, Nchi yetu imebarikiwa sana kuwa na hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba,Mapori Tengefu na Hifadhi za Jamii za wanyamapori ambavyo ni vivutio kwa utalii wa picha na pia uwindaji wa kitalii. Ili kuweza kuvitumia vivutio hivi kuongeza pato la Taifa, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

a) Kuongeza juhudi na mbinu za kisasa katika kutokomeza ujangili na biashara haramu ya wanyamapori hii ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya kujenga uwezo wa kupambana na ujangili pamoja na kuimarisha doria za mara kwa mara.

b) kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa wanyamapori walio hatarini kutoweka kama faru na tembo;

c) Kushirikiana na Mamlaka husika kubaini mbinu za kupunguza vifo vya wanyamapori wanaokufa kwa kugongwa na magari katika barabara zinazokatiza katika hifadhi zetu hasa katika hifadhi ya Taifa ya Mikumi ambako kwa wastani mnyama mmoja hugongwa kila siku;

d) kuongeza juhudi katika kusimamia sheria na taratibu ipasavyo kwa kuwashughulikia kikamilifu wote watakaokutwa na hatia ya ujangili wa wanyamapori hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kesi za ujangili zinasikilizwa haraka na kutoa adhabu kali kwa watakaokutwa na hatia.

e) kuhamasisha wananchi wanaoishi katika maeneo yanayopakana na hifadhi za wanyamapori kushiriki katika uanzishaji na usimamizi wa maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanayamapori (WMAs)

f) Kusimamia mipaka na maeneo ya mapori kwa lengo la kutatua migogoro iliyopo na inayoweza kujitokeza kwa lengo la kunusuru ikolojia, kulinda mazalia ya wanyama, mapito ya wanyama pamoja na vyanzo vya maji kwa ajili ya kuendeleza hifadhi na utalii nchini.

## 3.3 SEKTA YA MALIKALE

**Mheshimiwa Spika,** Malikale ni rasilimali za urithi wa taifa tangu enzi za wahenga wetu. Rasilimali hii ikiboreshwa ipasavyo itachochea utalii na kuchangia ukuaji wa uchumi na kukuza sekta ya elimu hapa nchini**.** Hivyobasi Kamati inaliomba Bunge kuitaka Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuongeza mapato na kuinua sekta ya Malikale:-

a) Kuainisha vivutio vya malikale pamoja na kuviendeleza, sambamba na kuimarisha ulinzi, kukarabati na kutunza maeneo yenye majengo ya Malikale kwa lengo la kuuenzi utamaduni wetu na kuvutia watalii kutoka katika maeneo mbalimbali nchini;

b) Kuendelea kukuza utalii wa ndani kwa kuyatangaza maeneo ya Malikale ndani na nje ya nchi kama vivutio vya utalii na maeneo ya kujifunza historia ya nchi yetu;

## 3.4 MAKUMBUSHO YA TAIFA

**Mheshimiwa Spika,** Makumbusho ya Taifa ni moja ya idara muhimu yenye kutunza kumbukumbu na historia ya taifa kwa ujumla kabla na baada ya kupata uhuru.Ni kivutio cha utalii na ni kielelezo muhimu katika kuinua kiwango cha elimu nchini. Cha kusikitisha zaidi Serikali inaisahau idara hii muhimu hivyo Kamati inaikumbusha Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuinua idara hii:-

a) Kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya ukarabati wa maeneo ya makumbusho ya Taifa
b) Kutangaza Makumbusho ya Taifa kama kivutio sambamba na vivutio vingine vya utalii; na
c) Kuhamasisha wananchi kuitambua, kuithamini na kuitembelea makumbusho ya Taifa kama hatua ya kukuza utalii wa ndani pamoja na kuongeza uelewa wa historia ya nchi yetu.
d) Kuendeleza Makumbusho ya Taifa kwa kujenga vivutio mbalimbali kama vile maduka, vyoo, migahawa kwa lengo la kuinua utalii na kuwavutia watalii wengi kutembelea.
e) Kuitangaza makumbusho ya Taifa hasa kituo cha Bonde la Oldivai ambacho ni chimbuko la historia ya binadamu wa leo.

## 3.5 SEKTA YA MISITU NA NYUKI

**Mheshimiwa Spika,** Idara ya misitu ni muhimu katika kuhifadhi mazingira, kurekebisha mfumo wa hali ya hewa, kupunguza mabadiliko ya tabia nchi, Kuhifadhi bioanuai, pamoja na kuhifadhi vyanzo vya maji. Pamoja na hayo, idara hii ikitunzwa kikamilifu itachangia ongezeko la ajira na kupunguza umaskini. Kufuatia fursa hizi Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuinua sekta ya misitu na nyuki;-

(a) Kuimarisha ulinzi katika misitu hapa nchini ili isivamiwe na shughuli za kibinadamu zisizoendelevu kama uvunaji haramu, ufugaji, uchomaji mkaa usio endelevu na kilimo zinazopelekea hali ya rasilimaliya miti kuwa duni;

(b) Kutangaza hifadhi za misitu asilia kama vivutio vya utalii ili kuongeza mapato yake;

(c) Kuanzisha mamlaka moja itakayokuwa na nguvu za kisheria kudhibiti matumizi ya rasilimali zote za misitu nchini;

(d) Kutoa mafunzo yanayohusu kuanzisha na kuendeleza misitu kwa wananchi wanaozunguka misitu ya hifadhi kwa lengo la kuimarisha ushiriki wa wananchi katika uhifadhi wa misitu na hifadhi za nyuki.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, nawapongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa mliokabidhiwa**.**

**Mheshimiwa Spika,** kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa wakati wa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Nape M. Nnauye, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Kemirembe Lwota, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mch Peter Simon Msigwa, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Boniface Mwita Getere , Mb - " -
5. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb - " -
6. Mhe. Jaffar Sanya Jussa, Mb - " -
7. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb - " -
8. Mhe. Khalifa salim Suleimani, Mb - " -
9. Mhe. Dr. Jasmine Tisekwa Bunga, Mb - " -
10. Mhe. Magdalena Hamis sakaya, Mb - " -
11. Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb - " -
12. Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb - " -
13. Mhe. Lucy Fidelis Owenya, Mb - " -
14. Mhe. Omary Tebweta Mgumba, Mb - " -
15. Mhe. Risala Kabongo, Mb - " -
16. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb - " -
17. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb - " -
18. Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb - " -

19. Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb - - " -
20. Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mb - - " -
21. Mhe. Flatei Gregory Massay,Mb - - " -
22. Mhe. Mbarouk Salim Ali,Mb - - " -
23. Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa, Mb - - " -
24. Mhe. Neema William Mgaya, Mb - - " -

**Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussen, Makatibu wa Kamati Ndugu Gerald Magili, Ndg Haika Mtui, na Ndg Jane Ndulesi kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii Fungu 69 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.



Nape Moses Nnauye, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA ARDHI,**

**MALIASILI NA UTALII**

21 Mei, 2018